# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara yaChukwani, Buyu,
70490 MjiniMagharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwanza kabisa. naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa rehema, kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, kwa lengo la kutekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, nachukua nafasi hii adhimu kwa moyo mkunjufu kabisa, kumshukuru Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, kwa kuendelea kuitumikia nchi yetu. Maendeleo endelevu yanaendelea kuonekana katika sekta ya kilimo nchini, Tunamuomba Allah ampe nguvu zaidi aweze kuzitekeleza vyema ahadi zote alizozitoa mbele ya wananchi wa nchi hii, wakati wa kampeni za uchaguzi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia inawapongeza kwa dhati Makamo wa Pili wa Raisi Mheshimiwa Hemedi Suleiman Abdulla na Makamo wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya, ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake ya kikatiba.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, shukurani pia tunazitoa kwako wewe binafsi Mheshimiwa Spika Zubeir Ali Maulid pamoja na wasaidizi wako akiwemo Naibu Spika, Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Wenyeviti wa Baraza, Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Mheshimiwa Abdalla Hussein Kombo kwa jitihada zenu katika kuliongoza Baraza hili tukufu kwa ustadi na weledi wa hali ya juu kabisa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Mheshimiwa Shamata Shaame Khamis, Katibu Mkuu, ndugu Ali Khamis Juma, Naibu Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini, wakurugenzi pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa jitihada kubwa wanazozichukuwa katika kuyapeleka mbele maendeleo ya kilimo nchini.

**Mheshimiwa Spika**,

Nachukua nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa kushiriki vyema katika kazi ya kupitia mapendekezo ya Bajeti hii kwa umakini na umahiri katika kutoa michango yao yenye lengo la kuhakikisha kuwa, sekta ya kilimo inaimarika na kuiletea nchi yetu maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena niwatambue kwa majina wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mwenyekiti
2. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Said Saleh Salim - Mjumbe
4. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Mjumbe
5. Mhe. Mihayo Juma Suleiman - Mjumbe

6. Mhe. Dkt. Mohammed Ali Suleiman - Mjumbe
7. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Mjumbe
8. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati hii inafanya kazi zake kwa kuratibiwa na makatibu watatu na msaidizi mmojaa mbaoni:

1. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi Katibu
2. Ndg. Asma Ali Kasim Katibu
3. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi Katibu
4. Ndg. Azmina Khamis Hamad Msaidizi

**Mheshimiwa Spika**,

Moja kati ya jukumu la msingi la Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ni kuchambua mapendekezo ya Serikali, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kila mwaka wa fedha, kama Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) ilivyoelekeza. Katika kulitekeleza jukumu hili,

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilikutana na Wizaraya Kilimo , Umwagiliaji, Mali Asili na Mifugo siku ya Jumanne ya tarehe 02/05/2024 na tarehe 07/05/2024 kwa lengo la kupitia, kujadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Hadi kufikia mwezi Machi 2024 Wizara ya Kilimo ilifikia asilimia **70%** ya makusanyo yake wakati mwaka 2023 kipindi kama hiki Wizara ilikua ipo katika asilimia **81%** katika makusanyo.

Hii inadhihirisha kushuka kwa mapato jambo ambalo kamati hatujalitatarajia.

Hivyo naiomba Wizara izidishe bidii na juhudi kwa kuwatumia wataalamu wake waliopo ndani na nje ya Wizara ili mambo yawe mazuri. Kwani ukusanyaji mzuri wa mapato ndio kila kitu katika ustawi wa Wizara.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia inachukuwa nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wake Mheshimiwa Rais Dkt, Hussein Ali Mwinyi kupitia Wizara yake inayoshughulika na mambo ya fedha, kwa hatua yake ya kuitengea Wizara hii bajeti inayotoa sura itakaoiwezesha Wizara kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Jumla ya shilingi **bilioni 5,704** zimepangwa kukusanywa na shilingi **bilioni 128.108** zimepangwa kutumika kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati sasa, napenda kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, maoni kuhusiana na bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kuzingatia programu kuu za Wizara hii kama ifuatavyo:

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa kazi nzuri inazoendelea kuzitekeleza katika kuiletea maendeleo sekta ya kilimo nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali imewekeza fedha nyingi katika kuimarisha ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji nchini.

Hivyo Wizara ya Kilimo inapaswa kuzidisha umakini katika matumizi ya fedha hizo kwa kusimamia ujenzi wa Miundombinu hiyo, kuhakikisha kwamba Miundombinu ya Umwagiliaji inayoendelea kujengwa, inakidhi viwango na thamani halisi ya fedha itakayotumika iweze kuonekana.Kwani kamati yako katika ziara zake za kawaida iliwahi kutembelea baadhi ya mabonde na kukuta hali sio nzuri.

Maji hayawafikii wakulima, utaratibu mbaya wa ugawaji maji katika mashamba pamoja na mitaro iliyojengwa inapoteza maji. Hivyo tunaiomba Wizaraya kilimo hali kama ile isije ikajirudia tena.

**Mheshimiwa Spika**

Wakati kamati yako inaipitia makadirio na mapato na matumizi ya Wizara hii kuna hoja mbalimbali ziliibuka ambazo kama zitafanyiwa kazi basi Wizara hii itatuletea tija kubwa. Hoja zilizoibuka ni kama vile matumzi mazuri ya vituo vya Kilimo kama Bungi na vyengine vingi ambavyo vimejengwa hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**,

Vituo hivi vilikua vikizalisha miche ya mazao ya chakula, kuhudumia wananchi na kukusanya mapato. Cha kusikitisha vituo hivi kwa sasa vipo katika hali mbaya na wafanyakazi waliopangiwa vituoni hapo hawana shughuli za msingi wanazozifanya.Tunaiomba Wizara ya kilimo irudishe shughuli vituoni humo ili Serikali yetu iweze kutanua wigo wa kukusanya mapato.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuhakikisha kwamba nchi inajiwekea hakiba ya kutosha ya chakula, Serikali kwa makusudi iliamua kujenga Maghala ya kuhifadhia chakula nchini kwa lengo la kuhifadhi baadhi ya vyakula ambavyo vinatumika sana nchini pindi vikiadimika sokoni viweze kutumika.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia imebaini kuna changamoto za kusafirisha mazao hali inayorudisha nyuma wakulima wetu. Utaratibu wa kutolewa vibali vya kusafirishia mazao itabidi ufanyiwe marekebisho kwani bado wimbi la wizi wa mazao ni kubwa na tusipokua makini tutashindwa kuwashawishi wakulima kuendelea na shughuli zao za kilimo nchini. Wizara iunde kamati ndogo ya kupambana na kudhibiti wizi wa mazao kwani utaratibu uliopo sasa wa kuwaruhusu masheha ndio watoe vibali bado ni tatizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Tunaiomba Serikali ianze kuyatumia maghala hayo hayo ya kuhifadhi vyakula ili ile adhama iliyokusudiwa iweze kutimia. Kwa upande wa Unguja Ghala limejengwa Kizimbani, kwa gharama ya shilingi Milioni **930,589,050** ambalo linakisiwa kuhifadhi tani **1500** za mazao. Na kwa upande wa Pemba ghala hilo limejengwa Dodeani kwa gharama ya shilingi Milioni **872,331,900** linalotarajiwa kuhifadhi tani **1000** za mazao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha **2024/2025**, Programu hii imetengewa jumla ya shilingi bilioni **101,485**. fedha ambayo imeongezeka ukilinganisha na fedha iliyotengwa kwa mwaka wa fedha **2023/2024**, ambapo ilikuwa ni jumla ya shilingi bilioni **78,201,262,000**.hii imetokana kwa ongezeko la miradi ya wafadhili. Wizara ya kilimo ina miradi **12** ila miradi saba **7** yote itatumika katika kuongeza nguvu katika programuu hii kwani lengo la kuhakikisha Wakulima wanaongeza uzalishaji ili nchi iweze kujikimu kwa chakula. Sekta ya Kilimo ni sekta mama ambayo imegusa moja kwa moja maisha ya wananchi hasa tukizingatia kwamba, wananchi walio wengi wamejiwekeza katika sekta hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati inaishauri sana Wizara ya Kilimo kuwa makini katika matumizi ya fedha hizi, ili kila shilingi itakayotumika iweze

kuonekana. Wizara inapaswa kuzingatia zaidi Sheria za Usimamizi wa fedha, Sheria ya Manunuzi na kusimamia vizuri Mikataba ya ujenzi katika miradi inayoendelea ili tija, ufanisi na thamani halisi ya fedha itakayotumika iweze kuonekana.

PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii utekelezaji wake unasimamiwa na Idara ya Misitu ikiwa na lengo la kusimamia misitu na kuhifadhi Wanyama pori pamoja na mazingira yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuitekeleza programu hii, Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Misitu imelenga kukamilisha utaratibu wa kuipandisha hadhi kwa baadhi ya misitu kwa upande wa Unguja na Pemba, kuimarisha ulinzi kwa kufanya doria katika maeneo ya misitu ya hifadhi na misitu ya jami na kufanya tafiti ili kubaini aina za wanyama pori ambao wanakaribia kutoeka.

**Mheshimiwa Spika,**

Wakati Wizara ikiendelea na mchakato huo, Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Misitu kuwashirikisha kikamilifu wananchi wenye mashamba ndani ya misitu hiyo kwa lengo la kuepusha migogoro kati ya wananchi hao na Serikali hapo baadae, kuharakisha utafti ili kunusuru wanyama pori ambao wanakaribia kutoweka pamoja na kudhibiti uharibifu wa misitu.

**Mheshimiwa Spika,**

Suala la uharibifu wa misitu kwa kukata miti kiholela nimeamua kulisemea kwa kina kwani tumeanza kushuhudia mabadiliko ya hali ya hewa katika maeneo mbali mbali Duniani ambayo yamesababishwa na shughuli za mwanaadamu. Hili suala la uharibifu wa misitu pia linaenda sambamba uhalifu ndani ya misitu yetu kwani tumepokea taarifa mbali mbali kua ndani ya misitu hiyi wanakutwa wananchi wakipika pombe za kienyeji ambazo

zimekatazwa nchini pamoja na kuficha baadhi ya vitu ambavyo vimeibiwa mitaani.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mujibu wa fedha hizi zilizotengwa tunaiomba Wizara ya kilimo ishirikiane na mamlaka za ulinzi na usalama ili kuweza kupambana na changamoto hii ambayo inawakosesha usingizi wakulima wetu hapa visiwani.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuitekeleza Programu hii, kwa mwaka wa fedha **2024/2025** Serikali imetenga jumla ya shilingi **bilioni 4.504** kati ya hizo shilingi bilioni **2.791** mishahara , shilingi million **530.00** kwa matumizi mengineyo na shilingi bilioni **1.183** kutoka kwa washirika wa maendeleo**,** fedha ambayo imeengezeka ukilinganisha na fedha iliyotengwa kwa mwaka wa fedha **2023/2024**, ambayo ilikuwa ni jumla ya shilingi **bilioni 3.457.**

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia hali hii, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuwaingizia kiasi hicho kilichotengwa kwa wakati, ili waweze kufanikisha yale yaliyopangwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kufungua milango katika kuendelea kutafuta wahisani na washirika mbalimbali wa maendeleo, wenye nia ya kusaidia katika sekta hii ya kilimo hasa tukizingatia Serikali imeruhusu uwekezaji katika maeneo yote nchini.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu ya Maendeleo ya Mifugo kupitia Programu yake ndogo ya Programu hii ina Programu Ndogo mbili za Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo, pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (ZALIRI).

Mheshimiwa Spika,

Miongoni mwa shabaha iliyoekwa katika program hii ni pamoja na Kufunga uzazi mbwa 50 na paka 350 ili kupunguza tatizo la wanyama wazururaji. Kamati yetu inaunga mkono suala zima la kupunguza wanyama wazururaji na tishio ila Tunaishauri Wizara yetu hii ya kilimo iendelee kuzitumia fedha hizi katika suala zima la kutoa Elimu kwa wafugaji ili waachane na ufugaji wa mbwa ambae tija yake ni ndogo na wajielekeze katika ufugaji wa mbuzi na kondoo. Kwa kufanya hivyo mifugo yetu itazidi kuengezeka na chakula kitaweza kutosheleza.Mheshimiwa Spika, kwa takwim ziliopo hivi sasa Zanzibar bado ni tegemezi katika suala zima la kitoweo, zaidi ya asilimia 80% ya nyama inatoka Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Spika,**

Mchinjio yetu yanakabiliwa na changamoto kubwa ya uchakavu wa majengo, mitaro ya kupitishia maji na utaratibu mbaya wa kutundika nyama wakati wa kuchinja, hali inayopelekea kiwango kidogo cha ukusanyaji wa mapato kwani wananchi wanashindwa kwenda kupeleka mifugo yao kwa ajili ya kuchinjwa.Kwa bajeti hii, tunaioba Wizara ikayafanyie ukarabati machinjio yetu ili yaweze kutuingizia kipato.

**Mheshimiwa Spika,**

Hatahivyo, Kamati yetu tunatoe pongezi kwa marekebisho ya chinjio la kisakasaka kwani kamati ilipopita hali ilikua mbaya ila kwa sasa mambo yamekua mazuri. Tunataka na machinjio mengine yakafanyiwe ukarabati.

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Kilimo inashindwa kutekeleza baadhi ya miradi iliyopangwa kwa wakati kutokana na Wizara ya Fedha kushindwa kuwaingizia fedha hizo kama zilivyoidhinishwa kupitia Baraza lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Kilimo ilipangiwa kutekeleza miradi kadhaa ikiwemo Mradi wa Ujenzi Machinjio ya Wanyama - Nzi Wengi Gando, Mradi wa Ujenzi wa Machinjio ya Wanyama Kisakasaka, Mradi wa Ujenzi wa Karantini ya Wanyama Kisakasaka, pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Josho la Wanyama – Donge. Jumla ya shilingi **bilioni 5** zilipangwa na kuidhinishwa kutumika kwa utekelezaji wa miradi hiyo katika mwaka wa fedha 2022/2023 lakini cha kusikitisha, fedha hiyo haikuingia hata robo yake.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nikujuulishe kua kwa mwaka huu wa fedha tunaoumalizia wa 2023/2024 bado miradi hii inasuasua kwavile haijaingiziwa fedha.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa muktadha huo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, kuangalia umuhimu wa miradi hii kwa maendeleo ya taifa letu, wakati huo huo wajitahidi kuingiza fedha zilizopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kukamilika kwa miradi mingi ya kimkakati nchini, kunatoa sura nzuri ya namna nchi inavyopiga hatua katika kujiletea maendeleo.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho kabisa, napenda kukushukuru tena wewe binafsi **Mheshimiwa Spika,** kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa niaba ya Kamati, pamoja na kuwashukuru wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kutenga wakati wao na kunisikiliza kwa wakati nikiwasilisha hutuba hii. Sasa wakati umefika niwaombe wajumbe wa Baraza lako, waipitie, waijadili na hatimaye waiunge mkono bajeti hii, kwa lengo la kumuwezesha Mheshimiwa Waziri kutekeleza yale yote waliyojipangia katika mwaka huu wa fedha unaokuja.

**Mheshimiwa Spika,**

Mimi binafsi na kwa niaba ya Kamati ninayoiongoza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha.

**Ahsante,**

…………………………………

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
Makamo Mwenyekiti,
Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo
Baraza la Wawakilishi
**Zanzibar.**